# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA UCHAGUZI YA MWAKA 2002

## YALIYOMO


| KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Ufafanuzi. |
| 3. | Kufutwa au kurekebishwa baadhi ya maneno. |
| 4. | Marekebisho ya kifungu cha 3. |
| 5. | Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 4. |
| 6. | Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 7. |
| 7. | Marekebisho ya kifungu cha 8. |
| 8. | Marekebisho ya kifungu cha 10. |
| 9. | Marekebisho ya kifungu cha 11A. |
| 10. | Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 12. |
| 11. | Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 13. |
| 12. | Kufutwa na kuandikwa upya kwa Sehemu ya Nne Sheria ya Uchaguzi. |
| 13. | Marekebisho ya kifungu cha 42. |
| 14. | Marekebisho ya kifungu cha 43. |
| 15. | Marekebisho ya kifungu cha 51. |
| 16. | Marekebisho ya kifungu cha 56. |

17. Marekebisho ya kifungu cha 63.

18. Marekebisho ya kifungu cha 64.

19. Marekebisho ya kifungu cha 68.

20. Marekebisho ya kifungu cha 70.

21. Kufutwa kwa kifungu cha 72.

22. Marekebisho ya kifungu cha 75.

23. Marekebisho ya kifungu cha 79.

24. Marekebisho ya kifungu cha 127.

25. Marekebisho ya kifungu 130(1).

26. Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 133.

**SHERIA NAM. 12 YA 2002**

**NAKUBALI,**

**{ AMANI ABEID KARUME }**
**RAIS WA ZANZIBAR**
**NA**
**MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**25th OCT, 2002**

# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA UCHAGUZI YA MWAKA 1984 PAMOJA NA MAMBO MENGINE YAHUSIANAYO NA SHERIA HIYO

---

Imetungwa na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Jina fupi na kuanza kutumika.

1.(1) Sheria hii itajuilikana kama Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Uchaguzi ya 2002, na itasomwa pamoja na Sheria ya Uchaguzi, Nam. 11 ya 1984.

(2) Sheria hii itaanza kutumika mara tu itakapokubaliwa na Rais.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa venginevyo:-

"Idara maalum" maana yake ni Idara maalum zilizoelezwa katika kifungu cha 121 cha Katiba.

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na marekebisho yake;

"Mtu mtegemezi" maana yake ni mama, baba, bibi, babu au mtoto wa kuzaa anayeishi na mpiga kura;

"Sheria hii" maana yake ni Sheria ambayo inarekebisha Sheria ya Uchaguzi ya 1984;

"Sheria ya Uchaguzi" maana yake ni Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 kama ilivyowekwa pamoja na kujumuisha marekebisho yote yaliyofanywa mpaka kufikia tarehe 17 Julai 2000.

*Kufutwa au kurekebishwa baadhi ya maneno.*

3. Neno "daftari" pamoja na tafsiri yake linarekebishwa na kusomeka kama ifuatavyo:-

"daftari" maana yake ni daftari la kudumu la wapiga kura linalotayarishwa na kutunzwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

*Marekebisho ya kifungu cha 3.*

4. Kifungu cha 3 cha Sheria ya Uchaguzi kinarekebishwa kwa kukifanya kifungu cha 3 kuwa kifungu cha 3(1) na kuweka kijifungu kipya cha (2) kitachosomeka kama ifuatavyo:-

"3(2) Kanuni, maelezo au matangazo yoyote yale hayatotolewa chini ya kifungu cha 3(1) ila kwanza ipatikane idhini ya Tume ya Uchaguzi."

*Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 4.*

5. Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa, na badala yake kuwekwa kifungu cha 4 kipya kama ifuatavyo:-

"Kuundwa kwa Tume ya Uchaguzi.

4. Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo fumo wake, wajumbe wake na utaratibu wake utakuwa kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba."

*Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 7.*

6. Kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa, na badala yake kuwekwa kifungu kipya cha 7 kama ifuatavyo:-

"Mkurugenzi wa Uchaguzi.

7(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi ambae atateuliwa na Rais kutonana na mapendekezo ya majina yasiopungua mawili kutoka kwa Tume.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa Katibu na mtendaji mkuu wa Tume.

(3) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yote atakayopewa na Tume kama ilivyoainishwa ndani ya Sheria ya uchaguzi.

(4) Kila Afisa Uandikishaji, Msimamizi wa Uchaguzi au Mtu yeyote ambae atashughulikia uchaguzi kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi atatekeleza kwa ukamilifu maelekezo yote atayopewa na Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

7. Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uchaguzi kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(1) Kifungu cha 8(1) kinafutwa na kinawekwa Kifungu kipya cha 8(1) kitachosomeka kama hivi ifuatavyo:-

"8(1) Tume itateuwa Afisa uandikishaji kutokana na sifa zitazowekwa na Tume na kila afisa uandikishaji ataeteuliwa atakuwa ni mdhamini wa eneo la uchaguzi aliloteuliwa."

(2) Maneno "kwa wadhifa au jina" yaliopo katika kifungu cha 8 (2) yanafutwa na badala yake yanawekwa maneno:

"kwa mujibu wa sifa zitazowekwa"

Marekebisho ya kifungu cha 10.

8. Kifungu cha 10 kinafanyiwa marekebisho yafutayo:-

maneno "wanaweza kuteuliwa kwa nyadhifa au kwa jina"

yaliopo katika kifungu cha 10(2) yanafutwa na badala yake yanawekwa maneno yafuatayo:-

"watateuliwa kutokana na sifa ambazo Tume wataziweka".

Marekebisho ya kifungu cha 11A.

9. Kifungu cha 11A(1) kinafanyiwa marekebisho katika maneno ya utangulizi kwa kukifuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Wakala wa uandikishaji.

11A(1) Kila chama cha siasa ambacho kina nia ya kuweka Mgombea kinaweza kumteua mwanachama wake mmoja ambaye ni mkaazi wa eneo hilo la Uchaguzi kwa kila Ofisi ya Uandikishaji ambaye atajulikana kwa wakala wa Uandikishaji ambae atashughulikia uandikishaji katika jimbo ambalo chama chake cha siasa kimeweka mgombea kwa madhumuni ya."

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 12.

10. Kifungu chote cha 12 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kipya cha 12 kama ifuatavyo:-

"Sifa za kujiandikisha.

12(1) Hakuna mtu ataeandikishwa kuwa mpiga kura ila awe ametimiza masharti ya uandikishaji kuwa mpiga kura kama yalivyoelezwa katika Katiba.

(2) Hakuna mtu atakayeandikishwa kuwa mpiga kura katika zaidi ya jimbo moja la uchaguzi au katika zaidi ya eneo moja katika jimbo.

(3)(i) Mtu yeyote ambae ni mkaazi wa kawaida wa Jimbo linalohusika ataandikishwa kuwa mpiga kura wa jimbo hilo.

(ii) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, mtu atahesabiwa kuwa mkaazi wa kawaida katika jimbo husika ikiwa:-

(a) ana makaazi ya kudumu na amekuwa akiishi katika jimbo hilo kwa kipindi cha miezi thalathini na sita mfululizo tangu kuanza kutumika kwa sheria hii na mpaka kufikia siku ya kupiga kura ; au

(b) anaishi katika jimbo hilo kwa sifa za kikazi; au

(c) ni mke alieolewa au ni mume alieowa na anaishi katika jimbo hilo mradi tu mume wa mke huyo au mke wa mume huyo kwa kadiri itavyokuwa atakuwa ni mkaazi wa kawaida; au

(d) ni mtu mwengine anaemtegemea mmoja au wote wa watu waliotajwa katika aya ya (b) na (c);au

(e) ni mwanafunzi anaekaa katika dakhalia inayotambuliwa na Serikali iliomo ndani ya jimbo hilo.

(4) Mtu mwenye mke zaidi ya mmoja atakuwa huru kuchagua makaazi ya kudumu kwa mke mmoja yeyote.

(5) Mtu atahesabiwa kuwa anasifa za kikazi iwapo:-

(a) ni askari, aliepewa uhamisho unaotokana na uajiri wake na inajumuisha Jeshi la wananchi wa Tanzania, Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi na Idara Maalum;

(b) ni mfanyakazi wa Serikali au Shirika la Kimataifa na amepewa uhamisho kufuatana na shughuli zake za kikazi.

(c) ni mke au mume aliyeoa au aliyeolewa na mtu mwenye sifa za utumishi na ambaye amehamia eneo jingine kutokana na kuhamishwa mume au mke wake.

(d) ni mtegemezi wa mfanyakazi aliyetimiza masharti ya aya (a), (b) na (c).

(6) Pale mtu yeyote alieandikishwa kwa mujibu wa Sheria hii akipoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura jina lake litaondolewa kwenye daftari la wapiga kura; isipokuwa kwamba jina halitaondolewa kwenye daftari ila kwa kufuata masharti ya Sehemu ya Tatu na Nne ya Sura hii au kutokana na uamuzi ya Hakimu au Jaji kwamba mtu huyo ametiwa hatiani kwa makosa ambayo yanampotezea sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura au kupiga kura.

(7) Mtu ambaye, kwa madhumuni ya sifa za ukaazi hana sifa za kuandikishwa katika jimbo lake la sasa wakati wa uandikishaji, anaweza kurejea na kuandikisha kuwa mpiga kura katika jimbo lake la zamani na atakuwa na haki ya kuandikishwa katika jimbo hilo bila ya kujali masharti yoyote yaliyomo katika kifungu hiki.

(8) Jukumu la kuthibitisha kuwa mtu si mkaazi wa kawaida katika jimbo fulani litakuwa juu ya mdai isipokua kwamba kifungu hiki hakiondoi jukumu la mtu anayetaka kuandikishwa kuthibitisha mbele ya Afisa Uandikishaji kuwa ni mkaazi wa kawaida wa jimbo hilo.

(9) Tume inaweza mara kwa mara kwa kutoa amri, kuweka taratibu kuelekeza na kufafanua jambo lolote linalohusiana na makaazi ambalo halikuelezwa kwa uwazi na kifungu hiki."

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 13.

11. Kifungu chote cha 13 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa, na badala yake kinawekwa kifungu kipya cha 13 kama inavyofuata:-

"Kuanzishwa kwa daftari la kudumu.

13(1) Kutakuwa na daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

(2) Daftari la Kudumu la wapiga kura litatayarishwa na Tume ya Uchaguzi mapema iwezekanavyo.

(3) Tume ya Uchaguzi itaweka katika kila Wilaya kumbukumbu sahihi za Madaftari ya Kudumu ya Wapiga kura wa kila jimbo. Kila Daftari la kudumu la wapiga kura litajumuisha majina ya Wazanzibari wote wanaostahiki kupiga kura katika kila jimbo.

(4) Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar, na Afisi Kuu ya Tume ya Uchaguzi Pemba zitaweka kwa pamoja madaftari ya majimbo yote ndani ya daftari moja la kudumu la wapiga kura wote wa Zanzibar.

(5) Kila daftari la kudumu la wapiga kura litaonesha –

(i) jina kamili la mpiga kura;
(ii) tarehe ya kuzaliwa;
(iii) pahala anapoishi;
(iv) nambari yake ya kujiandikisha;
(v) jinsia ya mpiga kura;
(vi) eneo lake la kupigia kura.

(6) Hakutakuwa na mtu mwengine yeyote ataeruhusiwa kupiga kura katika jimbo ikiwa jina lake halikuorodheshwa ndani ya daftari la kudumu la wapiga kura la jimbo hilo.

(7) Mtu yeyote ambae amehamia au anaishi katika jimbo chini ya kijifungu cha (3) (ii) (b) mpaka (e) ya kifungu cha 12 atakuwa na haki ya kupiga kura katika jimbo hilo

ambalo yupo baada ya kukamilisha utaratibu wote wa uhamisho kama utavyoelezewa na kanuni zitakazotungwa na Tume kwa ajili hiyo.

(8) Utaratibu wote wa daftari la kudumu namna ya uwekaji wake, idadi ya madaftari hayo matumizi yake na namna ya kuweka pingamizi itakuwa kama utavyoelezewa na kanuni zitazotungwa na Tume kwa ajili hiyo."

Kufutwa na kuandikwa upya kwa Sehemu ya Nne Sheria ya Uchaguzi.

12. Sehemu yote ya Nne ya Sura ya Pili ya Sheria ya Uchaguzi, inafutwa na badala yake kuwekwa ifuatavyo:-

"SEHEMU YA NNE
RUFAA, KUONGEZWA AU KUONDOLEWA KATIKA DAFTARI LA WAPIGA KURA

Kukata rufaa.

29(1) Mtu yeyote anaweza kukata rufaa kwa Hakimu wa Mkoa kutokana na:

(a) Kukataliwa kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura; au

(b) kukataliwa maombi yeyote yale yaliyofanywa chini ya kifungu chochote kile kuanzia kifungu cha 16 hadi 22 cha Sheria ya Uchaguzi; au

(c) kutokana na kukataliwa ukaguzi wa daftari; au

(d) kutokana na kupingwa kwa pingamizi alioiweka.

(2) kila rufaa katika sehemu hii itasikilizwa na kukamilika katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kukata rufaa; na kwamba mlalamikaji ikiwa hakuridhika, anaweza kukata rufaa zaidi Mahakama Kuu. Maamuzi ya Mahkama Kuu yatakuwa ya mwisho.

(3) Hakuna upande wowote utakaodai kulipwa gharama au fidia katika rufaa hizi.

Kuondolewa au kuongezwa ndani ya daftari.

30. Endapo jina la mtu ye-yote:-

(a) limekubaliwa na Mahkama kuwekwa katika daftari la kudumu la mpiga kura; au

(b) limeamuliwa na Mahkama kuondolewa katika daftari la kudumu la wapiga kura,

Afisa Uandikishaji, baada ya kupata amri kutoka mahakamani au kutoka Tume atachukuwa hatua ya kuliingiza au kulitoa jina hilo katika daftari la kudumu la wapiga kura."

Marekebisho ya kifungu cha 42.

13. Kifungu cha 42 cha Sheria ya Uchaguzi kinarekebishwa kama ifutavyo:-

(i) kwa kuweka maneno:-

"na kwa mgombea au wakala wa mgombea" baina ya neno "Tume" na maneno "kwa utaratibu" yaliopo katika kifungu 42(1).

(ii) Kuweka neno "baadae" mara baada ya neno "na" na kabla ya neno "Tume" mara tu baada ya kijifungu 42(1)(c).

(iii) Kwa kukifuta kijifungu cha (4) ya kifungu cha 42 na kuweka kijifungu kipya cha (4) kama ifuatavyo:-

"(4) Mgombea Urais atatangazwa kuwa mshindi, iwapo tu atapata kura nyingi zaidi halali zilizopigwa kuliko wagombea wenzake."

Marekebisho ya kifungu cha 43.

14. Kifungu cha 43 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Kupiga kura kwa mara ya pili.

43(1) Endapo katika Uchaguzi wa Rais mwagombea waliopata kura nyingi zaidi wamepata idadi sawa ya kura, basi uchaguzi utarudiwa kwa mara ya pili.

(2) Tume ya Uchaguzi kwa kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi itatangaza tarehe nyingine inayofaa ambayo haitokuwa zaidi ya siku arubaini tokea siku ya uchaguzi kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Urais na taratibu za upigaji kura kwa nafasi hiyo zitaanza upya"

Marekebisho ya kifungu cha 51.

15(1) Kifungu cha 51kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kukifuta kijifungu cha (1) na kukiandika upya kama ifuatavyo:-

"Wagombea na siku ya uchaguzi.

51(1) Tume itatoa tangazo katika Gazeti la Serikali likimaanisha siku ya uchaguzi ambayo haitopungua siku sitini na haitozidi siku tisini kuanzia siku ya uteuzi ya wagombea.

(ii) Kuwekwa kijifungu kipya cha 51(2) kama ifuatavyo:-

"51(2) Uchaguzi wote wa Zanzibar unaohusu Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani utafanywa siku moja ila pale tu ambapo imetokea dharura muhimu na inayokubaliwa na Tume basi uchaguzi wa jimbo au majimbo fulani unaweza kuahirishwa na Tume kwa kutoa matangazo katika vyombo vya habari hadi siku ya pili yake au siku nyengine yeyote itayopangwa na Tume.

(iii) Kwa kuvifanya vifungu vya 51(2) na 51(3) sasa visomeke 51(3) na 51(4) kwa mpangilio huo.

Marekebisho ya kifungu cha 56.

16(1) Kifungu cha 56(2) kinarekebishwa kwa kuweka maneno "Tume ya Uchaguzi na nakala kwa" baina ya neno "kwa" na "Mkuu".

(2) Kifungu cha 56(3) kinarekebishwa kwa kuweka kituo kidogo badala ya kituo kikubwa na kuongeza maneno yafuatayo mara baada ya kumalizika kwa sentensi ya kijifungu hicho kama ifuatavyo:-

> "mradi tu taarifa hizo za mikutano zipelekwe kwa Tume ya Uchaguzi na nakala ya taarifa hiyo kwa Mkuu wa Wilaya".

(3) Kwa kuweka kijifungu kipya cha (5) kama ifuatavyo

> "(5) Kwa madhumuni ya kijifungu hichi, Tume ya Uchaguzi inajumuisha Wasimamizi wa Tume ya Uchaguzi katika Wilaya inayohusika".

Marekebisho ya kifungu cha 63.

17. Kifungu cha 63 kinarekebishwa kwa kuyafuta maneno yote yaliopo katika mstari wa mwanzo wa kifungu hicho na badala yake kuandika maeneno yafuatayo:-

> "Msimamizi wa uchaguzi kwa kufuata amri na maagizo ya Tume ya Uchaguzi atatekeleza yafuatayo."

Marekebisho ya kifungu cha 64.

18. Kifungu cha 64 cha Sheria ya Uchaguzi kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kufuta vijifungu vya (1) na (6) ya kifungu cha 64.

(ii) Kwa kufuta maneno ya utangulizi katika kijifungu cha (3) ya kifungu cha 64 na kuyaandika upya kama ifuatavyo:-

"Kila chama cha siasa chenye mgombea wa urais kitateua mwanachama wake mmoja na mgombea wa uwakilishi na udiwani mwanachama wake mmoja atakayejulikana kuwa ni wakala wa upigaji kura kwa kila kituo cha upigaji kura katika Jimbo ambalo chama hicho kimeweka mgombea kwa madhumuni ya"

(iii) Kwa kuvitia nambari upya vijifungu vilivyobakia na kuwa 64(1), (2), (3), (4) na (5).

(iv) Kwa kufuta neno "mgombea angeweza" katika kifungu cha (5) ya kifungu cha 64 na kuweka maneno "kila chama cha siasa kinaweza".

Marekebisho ya kifungu cha 68.

19. Kifungu cha 68(3) (c) (iii) kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

(iii) hakutokuwa na nambari, alama yoyote au jina litaloandikwa juu ya kishina cha karatasi ya kura ambacho kinaweza kumtambulisha mpiga kura."

Marekebisho ya kifungu cha 70.

20. Kifungu cha 70(2) kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(1) kukifuta kijifungu (j) na kukiandika upya kama ifuatavyo:-

"70(2)(j) Askari polisi na askari wa aina nyingine ikibidi kwa ajili ya kuweka usalama katika kituo cha upigaji kura;"

(2) Kukifuta kijifungu (k)

Kufutwa kwa kifungu cha 72.

21. Kifungu cha 72 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 75.

22. Kifungu cha 75 cha Sheria ya Uchaguzi kinarekebishwa kwa kuongeza maneno yafuatayo mara tu baada ya kumalizika kwa sentensi kama ifuatavyo:-

" ila tu ijulikane kuwa Afisa wa Uchaguzi wa kituo hicho atamuagiza polisi aliyepo kukaa mwisho wa mstari wa wapiga kura waliopo pale muda wa kupiga kura unapomalizika ili kuzuia wapiga kura wanaokuja baada ya muda uliowekwa kumalizika wasiweze kupiga kura".

Marekebisho ya kifungu cha 79.

23. Kifungu cha 79 (1) kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(1) Kwa kukifuta kijifungu 79(1)(e) na badala yake kuweka kijifungu kipya kifuatacho:-

"79(1)(e) Askari polisi na askari wa aina nyingine ikibidi kwa ajili ya kuweka usalama katika kituo cha kuhesabu kura;"

(2) kukifuta kijifungu chote cha (i).

Marekebisho ya kifungu cha 127.

24. Kifungu cha 127 cha Sheria ya Uchaguzi kinarekebishwa kwa kuondoa maneno "Mkurugenzi wa Uchaguzi" baina ya maneno "kama" na "atakavyoamua" na kuweka neno "Tume".

Marekebisho ya kifungu 130(1).

25. Kijifungu cha 130 (1) kinarekebishwa kwa kuongeza kijifungu kipya cha 130(1)(c) mara tu baada ya kijifungu 130(1)(b) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:

"130(1)(c) kuweka utaratibu wa uandikishaji na wa pingamizi katika daftari la kudumu la wapiga kura".

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 133.

26. Kifungu cha 133 cha Sheria ya Uchaguzi kinafutwa na badala yake kinawekwa kifungu cha 133 kipya kama ifuatavyo:-

"Mafao ya Wajumbe wa Tume.

133. Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi watalipwa mishahara, maposho na mafao mengine kama itakavyoamuliwa na Rais kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina."

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 10 Oktoba, 2002.

{ KHAMIS JUMA CHANDE }
**KATIBU**
**BARAZA LA WAWAKILISHI**